

**JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA**



WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO



**HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI**

Unapojibu tafadhalii taja: M NH/CSO/TENDER/VOL.III/52/2021

24/02/2021

**TANGAZO LA MWALIKO KWA WAJASILIAMALI  
KATIKA ENEO LA HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI-  
UPANGA**

1. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ina maeneo mbalimbali ya huduma za kijamii zinazohitajika kwa ajili ya kuhudumia watu katika eneo la hospitali.
2. Hospitali inawakaribisha wajasiliamali mbalimbali kujitokeza ili kuomba kufanya biashara katika maeneo yafuatayo:

BUNDA NA.	ENEO	BIASHARA	IDADI
1	MTC	Saluni ya kiume	1
2	MTC	Biashara ya Miamala ya Fedha	2
3	NURSES	Fundi ushonaji	1
4	NURSES	Saluni ya kiume	1
5	NURSES	Saluni ya kike	1
6	NURSES	Stationary	1
7	NURSES	Biashara ya Miamala ya Fedha	2
8	NURSES	Huduma ya duka	1

3. VIGEZO VYA WAOMBAJI
  - 3.1 Awe na kitambulisho cha Taifa.
  - 3.2 Awe na leseni ya biashara husika.
  - 3.3 Katika Barua ya maombi mzabuni aweke bei ya pango atakayotoa kila mwezi.
  - 3.4 Kila mzabuni anaruhusiwa kuomba bunda moja tu.
  - 3.5 Asiwe mfanyakazi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili
4. Wafanyabiashara wanaweza kuyaona maeneo husika ya kufanya biashara katika eneo la hospitali siku ya Jumatatu tarehe 01/03/2021, muda wa saa nne asubuhi.
5. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja na nakala kivuli (copy) moja zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa **“Bunda Na..... uwekezaji biashara ya .....”**  
**Hospitali ya Taifa Muhimbili\_Upanga.** Siku ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni ni tarehe 5 Machi, 2021 saa nne kamili asubuhi katika ofisi ya Manunuzi na Ugavi, Hospitali ya Taifa Muhimbili, S.L.P 65000 Dar es Salaam.. Zabuni zitafunguliwa kwenye ukumbi wa mikutano wa hospitali siku hiyohiyo mbele ya wafanyabiashara au wawakilishi wao wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni.
6. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji wa zabuni, kwa hali yoyote ile zabuni hizo hazitakubaliwa.

**Mkurugenzi Mtendaji**  
**Hospitali ya Taifa Muhimbili**